# UTAMADUNI, MATUMIZI NA MISINGI YA LUGHA YA KISWAHILI

### *Matumizi ya Lugha*

Mwanadamu kaumbwa na utafishi baada ya kujazwa ubongo. Ubongo ndio chemchem ya mawazo yake na hojaji zake. Kwa hiyo, haja ya kutafuta kila akionacho na kutaka kujua kila asikiacho ni moja ya tamaa zake.

Itakuwa hapana la ajabu kwetu sisi tukijishughulisha kutaka kujua juu ya matumizi ya lugha yetu pamoja na misingi yake. Ingawa jambo hili si rahisi, kwa sababu lina vipengele vingi na kwa hali hiyo ufumbuzi wake unataka mtu awe na makini ya kutosha, hata hivyo juhudi za kitu hazitatutupa mkono, lazima tutapata japo kwa uchache wa baadhi ya mambo tuyatakayo.

Itatosha nikisema ya kwamba tatizo la lugha halikuuacha ulimwengu utulie bila kuushughulisha. Sababu kubwa ni kwamba lugha inachukuliwa kuwa ni kitu muhimu sana, kitu ambacho hukusanyisha sanaa zote kwa maelezo na kwa maandishi. Lugha ni chombo kinachotumiwa kwa kurakibishia fikira za kiumbe huyu na yule. Hivyo lugha ina maana sana katika maisha ya mwanadamu wakati anapokuwa yu hai.

Kila watu wana lugha yao. Wengine lugha zao ni kubwa, wengine za kadiri na wengine ni ndogo sana kiasi cha sehemu yao tu au ukoo wao, lakini juu ya hayo, kila watu huwa ni wajibu kwao kuishughulikia lugha yao. Wala hakuna watu wa lugha fulani ikawa wanaibeua lugha yao na kuitukuza lugha ya wengine kwa hiyari zao. Hivyo inaonyesha wazi kwamba kila watu huipenda lugha yao, na katika kuipenda ni lazima kuitafutia njia zake, misingi yake na sarufi yake.

Hali kadhalika Waswahili na lugha yao ya Kiswahili nao wanaipenda kikweli, wanaithamini na kuitukuza, kwa vyo vyote hawaachi kutaka kuijua na kuisema kwa mapana na marefu. Ndipo kukawa na hamu kubwa kwa Waswahili kuichagua lugha ya Kiswahili ili iwe ni lugha ya taifa lao na iwe ni lugha ya Serikali ya Wananchi wa Tanzania.

Jambo hili linatia moyo sana, na kwa kufuata usemi wangu uliotangulia inaonekana dhahiri kwamba Kiswahili chahitaji upambanuzi halisi ili watu wanaokitumia wakitumie zaidi ya hivi wanavyofanya sasa.

### *Historia ya Kiswahili*

Tukitaka kuwa wasemaji au waandishi stadi wa lugha yo yote, lazima kwanza tuijue lugha yenyewe, tujue asili yake, wasemaji wake, wenyeji ni wapi na inasemwa wapi, miko yake kama zilivyo lugha nyingine, n.k. Tukishayajua hayo ni wazi kwamba tutakuwa tumeijua historia yake japo kidogo.

Japo kuna mvutano mkubwa baina ya wataalam juu ya lugha hii ya Kiswahili kana ni ya Waswahili au la kwangu ni mvutano unaotokana na hali ya maumbile ya Kibinadamu yanayoruhusu hiyari ya mioyo. Uwanja waelimu ni mpana na ni katika upana huo kwamba mivutano kama hii hugundulisha vitu na mambo kadha wa kadha.

Hakuna wakati ambao wataalam wa Historia wametueleza kwamba Pwani ya Afrika Mashariki ilikuwa haina watu kabisa. Wala hakujaelezwa kwamba kulikuwa na lugha kadha na kadha kabla ya kuletwa Kiswahili. Kwa hivyo maoni ya watu wengi ni kuwa watu walikuwepo, waliishi na walikuwa wakisema, hivyo ni wazi kwamba ye yote mwenye akili atakubali kwamba msemo waliokuwa wakiutumia ulikuwa wa Kiswahili. Nasema ulikuwa wa Kiswahili sababu ndivyo ijulikanavyo kuwa lugha ya watu wa mwambao wa Afrika ya Mashariki ni Kiswahili.

Maneno ya Kiswahili ni ya kienyeji cha watu wa Mwambao; watu hawa ni Waafrika na matamshi yao ni ya Kiafrika. Kuna vitu viwili muhimu ambavyo vyahitaji kukumbukwa, navyo ni:

(a) Kwamba Kiswahili kimeundwa kinamna ya pekee hitilafu kidogo na Kiafrika kingine.

(b) Kiswahili kimegawa Kusini na Kaskazini sawa sawa, hivyo naona ufasaha wake unategemea zaidi maana ya maneno kuliko uzito wa maneno yasemwayo.

Kiswahili ni kimwambao na Kimwambao ni Kiafrika ikiwa ni Kibantu kama watu wengi wanavyopatia pa kuelezea haja zao. Ila jambo moja la maana sana ni kwamba, Kiswahili ni lugha ya watu wa mahali maalum ambao walianza kuishi tangu miaka elfu na elfu. Watu ambao ustaarabu wa lugha yao unatupa ushahidi wazi kwamba haukukubali kuchujwa. Ingawa Waswahili na Uswahili wao uliingiliwa na jumla ya jamii za aina kwa aina za ustaarabu bado mila na desturi za Kiswahili zimebaki mali ya Uswahilini. Kuna watu wasiosadiki kuwa Kiswahili ni lugha ya watu maalum wa asili ya Kiafrika na kusema ati ni lugha ya mchanganyiko kati ya watu wa pwani ya Afrika Mashariki na Wasafiri wa Bara Arabu. Mimi siafiki fikira za namna hiyo. Nawe msomaji sikuombei zikupitie. Fikira hizo ni za watu ambao kidogo wanayatazama mambo kwa mvutio wa upande wa "la", na kwamba hawaji huku kwenye upande wa "naam."

Kiswahili kingekuwa si cha asili ya Kiafrika, vitu vya asili ya umbo la mtu vingekuwa na majina ambayo ni ya kigeni na mengi yenye kufanana na ya lugha nyingine. Hii ni dalili ya kuonyesha kwamba kuna lugha ya pekee ya Kiafrika inayoitwa Kiswahili.

Yafuatayo ndiyo maelezo ya muundo wa (a) kwa ufupi:

(i) Kiswahili kinaunga kibantu, kikurshi au kinubi pengine na Kinegro hivyo msemo wake unahitilafu kidogo na msemo ambao ni wa Kibantu kitupu.

(ii) Kwa kuwa lugha ya Kiswahili ilitokana na watu waliokuwa wakikaa katika sehemu kubwa ya Ukanda wa Pwani, hivyo ni dhahiri kwamba inasemwa kwa hitilafu za maneno kwa kadiri ya sehemu zilivyokuwa zimeachana umbali wake.

Kwa hivyo mtu akiyachungua mambo haya mawili, zitamjia fikra za aina mbili mbalimbali na atapata kufahamu kuwa kama lugha hii isemwayo ndiyo Kiswahili; basi japo itakuwa na tofauti za matamshi na pengine za msemo, lakini watu wake wanaweza kufahamikiana na kwamba mila na desturi zao lazima ziwe moja. Na hivyo ndivyo ilivyo kwa Pwani yote.

Pili, kwa kuwa lugha hiyo inasemwa katika eneo refu sana na ambako kila kipande cha eneo fulani huwa kinapakana na watu fulani wa bara wenye msemo wa aina fulani vile vile, hivyo ni dhahiri kwamba kila kipande kinachukua athari ya matamshi ya kabila lililo jirani nacho. Kadhalika kwa muda wa karne kadha wa kadha kwani ilikuwa ndilo lango la kuingilia Afrika. Kwa vyo vyote, lugha za kigeni zilipenya na kutia mizizi katikati ya Kiswahili na hapo ndipo paletapo matatizo katika kukichambua Kiswahili.

Maneno ya Kiswahili na Matatizo yake:

(i) Kufahamu kuwa yanahukumiwa katika wepesi na uzito wa matamshi pamoja na maana ya neno au maneno.

(ii) Kuhukumu kuwa neno au maneno yana misingi ipi, kama ni ya Kiafrika hakuna tabu sana lakini kama ni ya kigeni yataka uangalifu. Tuchukue mfano wa *nyungwi, ngungu* na *nyuzi.* Maneno haya hayafuati tabia moja. Msemaji kama hajui maneno ya kila neno itakuwa vigumu kwake kuyatumia barabara.

Vile vile maneno kama Mswaki, msuluhivu na shajari; yakipambanishwa yanaleta tabu, kwa hivyo jambo lililo bora kabisa ni kufahamu maneno haya ya asili ipi na yanafuata taratibu zipi. Kwa kuwa lugha hii inajitegemea yenyewe katika sarufi yake muundo wa taratibu zake katika sarufi haupatani kabisa na lugha nyingi za Kibantu, na asilani haimo katika sarufi ya Kiarabu kuilazimisha kuwa katika sarufi za Kizungu ni kama kupika mchanyato wa ndizi mbivu. Bila kuuliza matokeo yake itakuwa si mchanyato bali ni uji au bokoboko la ndizi. Maneno ya Kiswahili hayapatani na maneno ya Kizungu, kwa hivyo ni vigumu kukubali kufuata taratibu na tabia za sarufi ya Kizungu. Hapa ndipo tunapopata uharibifu wa lugha. Tutazame mifano ifuatayo:

(i) Asipokubali atalazimishwa kisiasa.

(ii) Ataeleza kiualimu.

(iii) Sote tunaishi kijamaa.

Ukiuliza kwa nini watu wanatunga mafungu ya maneno ya namna hii? Jibu lao litakuwa hivi "naam hivi ndivyo ilivyo sarufi." Kwa hakika hapa

tunarudi kwenye mfano wa Kiswahili usemao: "Baada ya donda msumari wa moto." Jibu hilo linaonyesha kuwa mafungu hayo ni ya kufuata muundo wa Sarufi ya Kizungu yenye maneno "Politically" (kisiasa), "Educationally" (kiualimu) na "Communally" (kijamaa) ambayo huitwa *"adverbial"* au kielezi kwa Kiswahili.

Nadhani si vibaya kwa watu kutaka kuikuza lugha lakini, ni lazima ukuzaji wenyewe uwe ni wa manufaa, usiwe ukuzaji wa kufuja na kuifisha lugha. Kutazamwe maslahi ya watu katika msemo isiwe ni kutengeneza mambo ambayo yakitumiwa hayaleti manufaa bali huonyesha kuwa watu wanaiga kila lijalo. Msemo wa Kiswahili haukubali kutumia 'ki' katika kuunda fungu la maneno ambalo linaambatana na sarufi ya Kizungu katika neno KIELEZI.

***Maneno ya Kigeni***

Tunapozungumza Kiswahili yatupasa kukumbuka kuwa, tunazungumza juu ya maneno makarimu na watu wayatumiao nao ni wakarimu. Iwapo ni hivyo, bila shaka uwanja wao haukosi wageni na maneno mageni. Hivyo ndivyo, maneno ya Kiswahili yalivyopokea maneno mengi ambayo ni ya Wageni waliokuwa wakija huku tangu hapo kale. Maneno hayo yamejiingiza na kujieneza katika Kiswahili hata imekuwa ni vigumu kufahamu kuwa ni ya asili gani au ya upande gani.

Haya maneno ambayo yana asili ya kigeni yamejistamirisha sana katika Kiswahili, nayo ndiyo ambayo yanawafadhaisha watu wengi sana. Kundi hili lina tabaka tatu. Tabaka hizi zinagawanyika katika vikundi vidogo vitatu, cha kwanza:

(i) Kikundi cha kale.
(ii) Matukio na mwisho.
(iii) Kikundi cha kupita.

Kama ilivyoelezwa katika maelezo ya juu yaliyohusu utangu wa Waswahili na Kiswahili katika Mwambao, ya kwamba ni wa kale, pia na hao wageni wa bara ya Asia walikutana nao tangu hapo kale, hivyo maneno ya kigeni yalipokewa yakajieneza na yakaenea. Haya ndiyo maneno yaliyomo katika tabaka ya kale. Maneno hayo yamechanganyika yanawaghilibu baadhi ya watu.

Mifano ni kama maneno yafuatayo: Mwanadamu, sanduku, sauti, kata, sahani, buruza, karatasi, alhamisi, kaburi, meza, kasha, bahari, mizani, kaure, bedeni, sahihi, saini, hakimu, mara, safari, simadari—ringisha, soko, samaki, karamu, arusi, jukumu, sinia, hadithi, mashariki, magharibi, asali, sandarusi, sukari, guru, kitabu, kusema, hesabu, chakula, sigara, dhihaka, maiti, mwalimu, mtalaka na mengi mengineyo ya aina hii.

Maneno kama haya ndiyo ambayo huleta mgongano wa mawazo. Mgongano wa aina mbili, kwanza, kwa watu wanaofahamu kuwa haya ni maneno ya Kiswahili ambayo ni ya asili ya kigeni na mengi yao yakiwa ni ya

Kiarabu. Wao huleta fikira kuwa kumbe Kiswahili asili yake ni maneno ya Kiarabu. Kwa hivyo Kiswahili ni Kiarabu na kwa vyo vyote Waswahili wanatokana na vizazi vya mchanganyiko wa Waarabu. Watu hao tatizo lao ni kuwa hawafahamu kuwa karibu kila neno la asili ambalo laonekana ni la kigeni basi lina neno lake la kiasili ya Kiswahili, jambo kubwa ni kujifunza na kutafuta kweli ilipo.

Pili kuna baadhi ya watu ambao hawapambanui kuwa kuna maneno ambayo ni ya asili ya kigeni na ya asili ya Kiafrika, wao hutumia maneno yote kwa namna moja. Hao nao huharibu sana msemo wa Kiswahili kwa kuyatumia maneno kiasi wanachodhani ndivyo pasi kufahamu mbinu na utaratibu wake. Sasa mambo haya huleta mabishano, na lugha huwa haina raha. Fikira hizi zote mbili zaamulika kwa urahisi iwapo aliyenazo atakuwa na subira ya kusikiliza pamoja na kujifunza.

Hapa nitaonyesha mifano ya tendwa ya tatizo hili, ukichukua neno Mwanadamu huoni ugeni unatoka wapi, hili ni neno la Kiswahili pekee. Lakini tunasema "mwana" ni kimwambao lakini "Adamu," si jina la kawaida la watu wa Mrima, hivyo Adamu ni jina lililoletwa kwa mbinu za Kidini na kwa vyo vyote limeletwa na Waarabu. Tamko letu ni "mtu." Ukichukua neno Sanduku nalo pia si la Kiafrika, lakini liko Bweta au jamanda. Haya hayana uzito. Tuchukue neno kama "Sauti," hili ni la Kiarabu na hutumiwa hivi, "sauti hii ya nini? au hakutoa sauti hata kidogo?" Lakini unapokuja katika Kiswahili cha neno hilo, matumizi yake hubadilika, katika sarufi na Sanaa yake.

Mfano: *"Kelele"* au *"kwenzi."* Kelele, huhesabiwa katika wingi. Kwa hali hiyo husemwa, kelele hizi za nini, siyo "kelele hii kama itumikavyo katika sauti." Lakini ukwenzi ni umoja hivyo husemwa "ukwenzi huu au huo ulikuwa wa nini? Pia kuna kwenzi katika jumla ya wingi, ambazo hutumika hivi: "Watoto wanapiga kwenzi ya ambao (kama kwamba) walinda mtama."

Kwa kawaida watumiaji wengi hawana hofu juu ya kutumia maneno vibaya. Sababu ni kwamba hawapambanui asili ya maneno wayatumiayo na kujua huzungumzwa kwa taratibu gani. Hili ni jukumu la walimu ambao wanafundisha baadhi ya mambo ambayo wao wenyewe hawana hakika nayo wala hawaoni kuwa yafaa watafute sahihi ya mambo kabla hawajayabeleghesha. Ni vigumu kusema au kuandika Kiswahili kilicho fasaha kama neno au maneno bila ya kuwa na ikirari barabara. Kujua kwataka kujifunza. Yafaa tukubali kujifunza.

Kikundi hiki cha matukio nacho kina matatizo yake. Maneno ya kila lugha hufuata maendeleo ya nchi. Kwa hiyo watumiaji wa lugha yawapasa wazingatie na kuhifadhi mtiririko wa maneno ya vitu vipya. Lugha kama hii ya Kiswahili ina bahati kubwa sana kwani kila neno la kila kabila linaweza kujipenyeza na likakubaliwa. Hakuna ugumu wa kuchovyeka maneno ya kigeni ya vitu kadha wa kadha, lakini je vyafaa? Kwa kweli havifai, kwani kila lugha ina mipaka yake, ikiwa kila neno la kigeni litatiwa katika uwanja

wa Kiswahili bila uangalizi, baada ya muda fulani lugha itakuwa haijulikani inasemwaje au ni lugha gani. Kama mfano huu:

(i) "Sitaweza kwenda sababu lensi za macho yangu si barabara, nataka niripoti kwa Daktari anifanyie cheki tharale." au

(ii) "Oh! kongracheleshenni, nimefurahi sana kusikia kuwa dota wako amesaksidi katika exam yake ya midiwaifari" au

(iii) *"Bahati mbaya sana, mdogo wetu amekuwa dhaifu sana sana, yuko hospitali, Daktari asema ni kwa ajili ya Malnutrisheni, hivyo atahitaji vitu vya kumpa proteni mpaka hali yake iwe jadid murtade. Pia asema taka kumjengea nguvu ya kumongezea kabohaidreti na Oksijeni" ili awe shebashi barabara.*

Baa kama hilo ndilo ambalo watu wanajitahidi kulisogeza. Hii ni kwa sababu kuna urahisi mtupu katika Kiswahili wa kupokea neno la aina yo yote mradi litaandikwa kwa abjadi za kutamkika Kiswahili. Kwa hali yo yote, mwendo kama huo baada ya miaka ishirini Afrika ya Mashariki itakuwa inatumia lugha isiyo jina.

Sasa tuwatazame watu wa tabaka ya mwisho—*Kikundi cha Kupita*. Watu wenye mori wa kufuata sehemu hii, huwa wanapoteza wakati wao bure, vile vile huwa ni hatari, kwa sababu fungu hili ni la vijana zaidi ambao aghalabu hujiundia maneno kila siku katika kila mtaa na kila nchi.

Maneno yao huwa ni ya kufuata mazungumzo. Maneno hayo hayafai kuzingatiwa sana kwa sababu hutumika kwa haja na wakati maalum. ukimalizika basi neno au maneno hayo humalizika. Kuna watu ambao hudhani kuwa kupata maneno kama hayo ni kuchuma na kwa hali hiyo hufanya juhudi ili yaenezwe.

Katika kutahadharisha ili tusiende na kwenda mwendo kama huo, imekuwa hapana budi kueleza kinaganaga ubaya wa mtindo wa kufuata maneno ya muda. Maneno ya muda aghalabu hayana maendeleo wala hayana maana nzuri. Ni maneno yasemwayo kwa haja, haja ikishapita basi na neno huwa limetoka raha yake kabisa. Tutazame mifano ifuatayo (1) "E bwana tangulia mie ninakwenda kushika kidogo". (2) "Siku hizi unafuga nyati ndio? Hana akili anataka mienge miwili ya kazi gani? (3) Ndio tabia ya mmatumbi hakawii kugeuza nia."

Kuna maneno madogo mengi sana ambayo hutumiwa na watu fulani kisha hupotea. Maneno haya hayana sahihi wala hayadumu katika jamii za watu ingawa aghalabu, huingia kwa nguvu sana na baada ya muda hughibu. Kama maneno hayo yote yanakubalika na kutiwa katika vitabu, ingekuwa hakuna maana hasa ya neno kama *kushika,* ambako watu wa muda wanalipa maana ya *kula.* Fungu la pili, *nyati* wao wanalipanga maana ya *mwanamke.* Neno *mwenge,* ati ni *shilingi moja.* Mmatumbi hapa maana

yake *mtu mweusi.* Na kwa hakika sana haya yamekwishapita au nusu yanamaliza enzi yake. Basi ikumbukwe kwamba watu wanaodhani kuwa kusikia maneno ya vijana ambayo huja na kutoka kwa muda ni kuchuma kwa msamiati wa lugha halisi, hao wanapotea.

Kwa vyo vyote kuyashikilia maneno kama haya ili yapangwe katika jumla ya maneno ya kutumiwa katika Kamusi au baadhi nyingine ni hatari ambayo yahitaji kuchunguzwa. Na mara nyingi ni matamshi yasiofaa kwani sana huwamo matusi na vineno vya kebehi.

***Udakiliaji wa Maneno***

Hali ya Kiswahili inakubali kuchukua maneno ya aina nyingi. Hivyo kuna baadhi ya watu ambao hutegemea kusikia neno au maneno na kutaka kuyatumia. Mwendo huo ni wa hasara sana tena mbaya mno, aghalabu watu wa namna hiyo huwa ni wepesi kwa kusikia maneno mbalimbali na mara kuanza kuyatumia baada ya kuyasikia maana zake. Hawashughuliki kutaka kujua namna ya matumizi yake, pia hata maana huwa haikamiliki. Mtindo wa watu wa tabaka hii aghalabu ni wa ubishi na uharibifu wa msemo, kwa sababu mwenye kusikia na kutumia huwa ana hakika kwamba amepokea kitu muitamadi, kwa hivyo hawezi kusikia la mtu mwingine.

Kwa mfano tuchukue maneno machache ambayo pengine mtu ameyasikia na akayazingatia kwa haraka; ikawa hakuyatalii barabara, bali mara alianza kujiona kuwa keshajua na kuanza kutumia kama hivi:

Neno *makala,* kwa maana ya maandishi, mtu anasema makala hii haikuandikwa vizuri. Hilo ni kosa, kwa sababu haisemwi ni *"makala* hizi, bali ni *makala haya."* Kuna baadhi ya watu ambao bila kuuliza hudhani kuwa "makala" huwa na umoja na wingi.

Vile vile neno: Guu—maana yake ni mguu wa kawaida, japo kuna mfano usemao "Asiyesikia la mkuu mwishowe huvunjika guu." Hii haina maana ya kuwa guu ni mtu wa kawaida, na tangu asili ya lugha hii mguu uliitwa ondo au 'guu' ambapo watu wa Mvita wao wanatumia "guu" hawana *mguu.* Sisi ndio tulio na mguu na miguu. Lakini kwa mwenye kusikia na kudakia bila kutafuta mambo yalivyo, huwa hakubali kufuata anavyoelezwa; yeye hudhani kuwa guu ni mali ya mguu, au labda guu ni mguu wa tende au mguu uliovimba. Mfano mwingine ni wa neno "uturi" yaani "manukato." Mara mtu akishasikia kuwa kuna neno uturi—basi hulidaka, na akatumia "uturi hili halinukii vizuri." Hivyo sivyo. Uturi ni tamko lenye asili ya Kiarabu na Kiajemi kwa maana ya manukato. Katika Kiswahili neno uturi linahukumiwa kwa urefu. Husemwa "uturi huu," siyo kwa kuwa ni harufu basi iitwe "uturi hii" la. Lakini haya yote hutokea kwa watu ambao wana harara ya kusikia na kudakia maneno pasi kuchungua au kuuliza maana na taratibu za matamshi na matumizi ya kila neno.

Tabia hii inaharibu sana Kiswahili kwa vile mara neno au maneno yakitumiwa ndivyo sivyo huwa yanaeneza ugonjwa na kutokuwa sawa kwa lugha. Hasa inapotokea kuwa mtumiaji ni mwalimu wa shule. Athari yake

huwa ni kubwa sana. Baada ya miaka michache lugha huwa imepotezwa kwa kiasi ambacho mtu atakuwa hawezi kunyoosha lo lote tena.

### *Visa vya Maneno*

Tamko hili la visa vya maneno linaweza kumfanya msomaji asifahamikiwe na maana yake lakini hasa maana yake ni sawa sawa na kusema:

"Ugumu wa kutambua mabadiliko ya maneno." Kwa nini basi nimeyaita visa vya maneno? Kwa sababu maneno ya Kiswahili yanamdhihirikia mtu katika hali ya visa visa kwani husikika kuliko tabia kama:

(i) Tabia ya Utishaji.
(ii) Tabia ya Uthakili.
(iii) Tabia ya Kawaida.

Katika ramsa hizi mtu anawajibika kutuliza makini yake wakati wa kutumia lugha hii ili aweze kuhukumu neno baada ya neno na kufahamu kila neno linafikia wapi. Waandishi wa kigeni wamejitahidi sana kuandika na kufundisha lugha hii ya Kiswahili lakini kwa kadiri ya jitihada zao walizofanya hawakuweza kufaulu barabara kugundua baadhi ya siri hizi. Si lawama kubwa kwao maana lugha yenyewe si yao, kiasi walichofanya wanastahili sifa ya pekee.

Watu wameweza kutunga sarufi za kigeni katika Kiswahili. Ninasema sarufi za kigeni kwa sababu njia za sarufi hizi si njia zile ambazo ndizo hasa wanazozitumia watumiaji wa Kiswahili. Ionekanavyo ni kwamba Wazungu wametafsiri maneno ya sarufi za lugha na kuilazimisha lugha ya Kiswahili ifuate Waswahili watake wasitake lazima iwe ndivyo hivyo. Si vizuri kusema kuwa watu hawa walifanya vibaya. Tukitazama tutaona walifanya jambo la maana, isipokuwa hawakutia maanani wajibu wa wasemaji wa lugha hii na kanuni za lugha waisemayo. Bali walizingatia ile hali na tabia na sheria za lugha zao na kuzifanya ziwe ni za Kiswahili. Pamoja na jitihadi za kupenyeza elimu ya lugha na siasa na uchumi, watu hawa wameweza kuwajaza wenye chao maelezo mazuri mpaka *yakawabwikia* ikawa hakuna anayetanabahi tena juu ya uzuri na upana wa Kiswahili.

Hapa ndipo nionapo mimi kuwa pamepitishwa hiyana ambayo tasiliti yake imewafanya watu wengi wasiofahamu sheria za lugha yao wasizifuate njia za usemaji wao wala wasithamini lugha yao. Badala yake huisema na kuiandika vyo vyote vile mtu aonavyo ndivyo. Tukio hili ndilo lililokuwa chanzo cha kutafuta mantiki katika lugha ya Kiswahili.

Sasa tutazame visa vya maneno ya Kiswahili vilivyo na ni vipi? Visa hivyo ni mabadiliko ya maana ya maneno kwa matamshi na sauti. Kwani kuna maneno yanayoonekana kuwa na tabia ya ukubwa na ya kutisha lakini maana yake huwa ni mepesi na rahisi. Katika hayo ambayo hayana shaka sana ni yale yaanzayo na silabi za G. J. na K. lakini kuna sababu za kutosha za kuyatoa katika uzito na utishaji wake, pindi iwapo tunataka kuelekeza usemaji wetu kwenye sheria zetu. Kwa mfano Ganzai, Gawadi, Jini, Jaji, Korosho, Kisu.

Halafu kuna yale ambayo yakitamkwa yanasikiwa kama kwamba kunatajwa kitu kilicho duni, chepesi, laini; lakini nayo pia yanahitaji kuchungwa kwani kama hakuna uangalizi basi hutumiwa kinyume cha taratibu za usemaji. Kwa mfano: Kibibi, kichipukizi, maiti, au chane. Tabia ya kawaida ndiyo iliyo na mizungu zaidi kwani maneno yake aghalabu hayaonyeshi taratibu zo zote kwa mfano: wangwa, kozi, onyo, shundishundi, embe, hoho na kadha wa kadha.

Matumizi ya aina hii ya maneno huwa hayafuati taratibu maalum balı kwanza lazima msemaji awe anafahamu maana ya jina au neno analolisema ndipo aweze kulichunguza hadhi yake kama linavyohusika.

Sasa tuchukue mifano ya maneno yote tuliyoyaonyesha kutoka katika tabaka za tabia za sauti za maneno. Tuanze na tabia (i) Ganzi, gawadi, jini, korosho na kisu. Majina haya yote yanatamkwa katika sifa za uzito, nayo yangeelekea kutumiwa kama hivi: ganzi, hili, na kadha wa kadha lakini haiwi hivyo sababu ganzi si dude ni hali ya ufishaji wa nguvu za neva, hivyo hii gawadi ni hali ya mtu, na mtu hawezekani awe *hili* bali ni *huyu*. Jini ni mahuluku mwenye umbo la nuru hivyo huwa ni huyu, jaji ni mtu mwenye uwezo wa kuhukumu na anahukumu, basi ni huyu haiwi jaji hili. Korosho japo ni tunda lakini haisemwi koroshi hili. Vivyo hivyo, kisu hakiwi *hili* bali *kisu hiki*.

Katika tabia ya (ii) matamshi yanaonyesha uthakili; kama vile kibibi, kichipukizi, maiti na chane.

Kibibi, ni jina la cheo cha mtoto wa mtu mkubwa. Ni sawa na mtoto wa kike wa Mtemi au Mangi. Hivyo hawi Kibibi *hiki*, bali ni *huyu*. Liko neno la kibibi ambalo linachukua uthakili wake, nalo ni lile la kibibi na andazi yaani kitu cha kuliwa. Vile vile kichipukizi huwa ni kizazi cha mtu kitokacho katika uzazi uliopita au upitao na huwa ni huyu au hawa. Maiti ni mtu hivyo hawi *hii* bali ni *huyu* kama vile tutumiavyo katika marehemu. Kadhalika chane, haiwi hiki au huyu bali huwa *chane hizi* n.k.

Tunapoingia katika visa vya mwisho vya (iii) tabia ya kawaida, hapa yataa kuzingatia kwamba kutumia Kiswahili cha kigeni, yaani kilichoendelezwa na Wazungu bila kutahadhari na kuzingatia taratibu za usemaji wa Kiswahili halisi ni kupotea. Mfano: kozi, onyo, shundishundi, embe, hoho, kozi ni ndege, hivyo ni huyu kama vile huyu ni kozi si mwewe, bali iwapo tunammithilisha na mwanadamu, huwa hili; kama vile "rafiki yako sasa si mtu tena limekuwa kozi." Hapa tunatoa maana ya unyang'anyi alionao, na ni kawaida ndege au mtu hupokea ukubwa wa visa vyake. Onyo ni tukio la kumfahamisha mtu hali ilivyo. Hali hiyo inakwenda na uzito wake ndipo inapotumika na neno hili; kama vile; amepata onyo kali. Shundishundi ni ndege mkubwa kuliko ndege wengine wote isipokuwa mbuni. Huyu hawi katika sheria za ndege, yeye anaathiriwa na tamko lake. Kwa hali hiyo, shundishundi huitwa shundishundi hili hasemwi huyu. Sawa sawa na bundi. Ajabu ni kwamba tukitumia hali ya uainisho wake twamwita huyu na hawa, lakini tunapotaja jina lake sheria ya sauti ya tisho inasimama pale pale, hivyo shun-

dishundi huwa hili kadhalika na bundi. Tukumbuke kwamba hakuna tatizo iwapo utasema, "huyu ni bata, likichinjwa ni zuri sana kwa chakula." Hoho ni pilipili. Hapa hoho haigeuki ikawa "hoho hili" wala hatusemi hoho baya japo tamko lake linajipa uzito na utishaji. Lakini fahamu ya kwamba twaweza kusema mabata haya, mapilipili haya, madege haya, iwapo tuna madhumuni ya kuzungumza juu ya sifa za ukubwa.

Kwa muhtasari, yafaa kukumbukwa kuwa kuna shuruti maalum ambazo zinamtaka msemaji wa Kiswahili azijue na azitumie. Watu wasijifunze sheria za lugha nyingine halafu wazigagamize katika lugha ya Kiswahili. Shuruti ni kielekezo cha lugha yo yote iwayo. Kwa nini kwingine ziheshimiwe na katika Kiswahili, zisiheshimiwe?

*Sarifa*

Hii ni fani ambayo watu waliotunga sarufi ya kigeni hawakuitumia au hawakuijua au waliona itawacheleweshea kazi zao. Hakika haiwezekani kutunga sarufi ili kuongoza lugha bila kutumia fani hii ya sarifa. Fani hii ndiyo inayojulisha uwezo wa msemaji au mwandishi juu ya neno moja au mawili na jinsi yanavyohusiana. Kwa jumla sarifa katika lugha ndicho chombo ambacho kinanyoosha usemi kwa hekima na kutambulisha asili ya kila neno na jinsi lilivyopatikana pamoja na maana kadha wa kadha kwa kufuata jinsi linavyosarifiwa. Kwa ufupi maana ya sarifa ni matumizi ya maneno katika mabadiliko ya sarufi na nahau. Kwa mfano; neno *Kuzaa*—asili yake ni *kuvyaa.* Hivyo twapata uzazi, mzaliwa, mzao, mzazi, mzalishaji, mvyausa, uvyauso, mvyele, mvyeleo, kizalia, n.k. Haya yote yamesarifika kutoka katika neno kubwa moja la asili ambalo ni *kuvyaa* au *kuzaa.* Hii ni moja tu ya fadhili za sarifa tukiacha jumla ya kazi bora za kuinyoosha lugha katika fani ya sarifa ambayo pasi hiyo sarufi zetu hazikamiliki.

## UFUNDISHAJI WA VITENDAWILI

Mazungumzo haya yalitolewa tarehe 1 Aprili, 1977 katika Semina ya Waalimu wanaofundisha Kiswahili katika Shule za Sekondari, Mikoa ya Dar es Salaam na Pwani; iliyotayarishwa na Taasisi ya Elimu na kufanyika katika Shule ya Sekondari ya Forodhani, Dar es Salaam.

*Utangulizi*

Ndugu Mwenyekiti na Ndugu Waalimu, naomba kwanza kuwashukuru wote kwa kuniruhusu na kunipa nafasi hii ya kuongea nanyi. Nafasi ya mwalimu wa kawaida kama mimi kuongea na hadhara ya waalimu kama hii mara nyingi ni haba sana. Kwa hiyo inapotokea kwa mtu wa aina yangu, huwa anawajibika kushukuru maridhawa.

Pamoja na shukrani hizo lakini Ndugu Waalimu lazima niseme